

# TAARIFA YA MAADHIMISHO YA WIKI YA MAJI 2017

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA.

### **“MAJI SAFI NA MAJI TAKA PUNGUZA UCHAFUZI YATUMIKE KWA UFANISI”**

#### 1. MAJI VIJIJINI

Tarehe 16/03 hadi tarehe 22/03 ya kila mwaka huwa ni wiki ya maadhimisho ya wiki ya maji yenye kilele chake tarehe 22/03 ambayo ni siku ya maji duniani. Mwaka huu maadhimisho haya yalibeba ujumbe usemao **“maji safi na maji taka punguza uchafuzi yatumike kwa ufanisi”**.

Aidha katika kuadhimisha wiki hii kwa vijiji ambayo kwa sababu zilizo juu ya uwezo wetu hatukuweza kufikia moja moja tulituma barua kwa watendaji wa kata zote ili wawashirikishe wananchi katika kata zao kuadhimisha wiki hii. Na kuwaomba watutumie taarifa baada tu kilele kuisha.

Halmashauri ya wilaya ya Kwimba tuliadhimisha kama ifuatavyo.

Tarehe 16/03/2017 tulizindua maadhimisho ya maji katika kijiji cha sumve kwa kupanda miti katika kisima kirefu kinachotoa huduma kijijini hapo, baadae tulikutana na serikali ya kijiji na kamati ya maji kwa shughuli ya uelimishaji kuhusu sera ya maji na usafi wa mazingira. Mgeni rasmi katika uzinduzi huu ni ndugu Eng Warioba Sanya mhandisi wa maji ofisi ya mkuu wa mkoa wa mwanza. Zoezi hili liliendelea katika vijiji vya Ilula, Kibitilwa, Hungumalwa na Ishingisha.

Tarehe 17/03/2017 maadhimisho ya wiki ya maji tuliyafanya katika shule ya msingi Igoma na shule ya sekondari Bujiku Sakila kwa kuelimisha wanafunzi na waalimu pia kuhusu usafi wa mazingira na usafi binafsi kwa kushirikiana na mwalimu wa afya mashuleni na afisa afya wa wilaya. Pia shule zilisisitizwa kuunda vikundi vya afya na maji yaani school water and sanitation hygiene clubs(SWASH)

Tarehe 20/03/2017 maadhimisho ya wiki ya maji tulifanya katika vijiji vya Kishili, Mwabilanda na Ilumba kwa kupanda miti katika vyanzo vya maji na baadae kukutana na serikali ya kijiji na kamati ya maji ya kijiji husika kwa uelimishaji kuhusu sera ya maji na usafi wa mazingira pia

uhamasishaji wa uundaji na usimamizi wa vyombo vya watumia maji kwa vijiji visivyokuwa na kamati kwa mujibu wa sera ya maji.

Tarehe 21/03/2017 wakati vijiji vingine na halmashauri vikiendelea kuadhimisha wiki hiyo Mhandisi wa Maji mmoja, Fundi sanifu mmoja na Msajili wa vyombo vya watumia maji walisafiri kuelekea Ukerewe kushiriki kilele cha maadhimisho ya wiki ya maji tarehe 22/03/2017 ki-mkoa

Tarehe 22/03/2017 kilele cha wiki ya maji kilifanyika katika wilaya ya Ukerewe kwa kuweka jiwe la msingi katika mradi wa maji malegea, mgeni rasmi katika shughuli hii ni mhe mkuu wa mkoa wa mwanza, John Mongela ambaye hakuhudhuria nafasi yake ilishikiliwa na mwenyekiti wa halimashauri ya wilaya ya Ukerewe mhe. George Matera Nyamaha. Pamoja na maadhimisho haya mgeni rasmi aliwakumbusha wananchi wa Ukerewe na wageni waalikwa wote juu ya vita kali ya madawa ya kulevya na kuwakumbusha wazazi juu ya wajibu wao kwa watoto.

#### 1. MAJI MJINI

Katika kuadhimisha wiki hii ya maji mamlaka ya maji mjini Ngudu ilifanya mikutano 7 ya wadau wa maji katika mitaa ya Kakora, Ngumo, Ngudulugulu na Bugakama. Kuhamasisha wananchi umuhimu wa kutumia maji safi na salama na faida za kuwa na mfumo wa maji majumbani, ili kufanikisha zoezi hili mamlaka ya maji mjini Ngudu iliweka punguzo la gharama ya kuunganishiwa maji majumbani kwa wateja wapya na wateja waliyositishiwa huduma hii awali walipunguziwa faini zao.

#### MAFANIKIO

Katika maadhimisho ya wiki ya maji mwaka huu 2017 tumefanikiwa kupanda miti 151 katika kijiji cha Sumve na miti 6 katika kijiji cha Ishingisha, Ilula+ Kibitilwa miti 12, Kishili miti 6, Mwabilanda miti 6, Ilumba miti 6.

Jumla ya wateja kumi (10) waliunganishiwa maji katika wiki hii na wengine wanaendelea kuunganishiwa kwa hilo punguzo maalum.

## CHANGAMOTO.

Baadhi ya watendaji kususia maadhimisho haya aidha kwa makusudi au kwa kutofahamu faida ya wiki ya maji katika jamii yao.

Ukosefu wa rasilimali fedha inafanya maadhimisho haya kuwa magumu na kutofikia kila kijiji na kufanya watumishi wasiyachukulie uzito unaofaa kama hapo awali ambao halmashauri ilikuwa inatoa fungu japo kidogo kwa ajili ya posho na viburudisho katika maadhimisho ya wiki hii.

## USHAURI

Maadhimisho haya ya wiki ya maji ni muhimu kwa ajili ya watu kuifahamu sera pia kuifanya hii miradi michache tuliyonayo kuwa endelevu nashauri serikali irudishe sherehe hizi katika umuhimu wake kama awali kwa kuweka fungu japo kidogo kwa ajili ya kufanikisha wiki hii kikamilifu kama ilivyokusudiwa wakati inaazimiwa.

Hizi ni baadhi ya picha ya matukio ya wiki ya maji 2017



Figure 1: Eng warioba akishiriki kupanda miti kijiji cha Sumve



Figure 2: mgeni rasmi na watumishi wa h/m ya kwimba pamoja na wenyeji wa sumve katika utambulisho baada ya kuwasili katika chanzo.



Figure 3: uelimishaji Sumve na upandaji miti na uelimishaji Ilula + Kibitilwa.



Figure 4: uelimishaji S/M Igoma na S/Sek Bujiku Sakila.

## Naomba kuwasilisha